

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO


NAMBA ZA SIMU

MKUU WA SHULE : 0753-979716/0714979716

MAKAMU MKUU WA SHULE : 0717-435450

WALIMU WA TAALUMA : 0664-6417432

: 0746-205972



SHULE YA SEKONDARI YA  
WAVULANA BUSOKELO  
S. L. P 02 TUKUYU

KUMB NA. BDC/BBSS/ADM:1/2

12.12.2020.

MZAZI/ MLEZI WA MWANAFUNZI \_\_\_\_\_

S. L. P \_\_\_\_\_

**MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WAVULANA BUSOKELO,  
ILIOPO KATIKA HALMASHAURI YA BUSOKELO MKOA WA MBEYA**

**1. UTANGULIZI**

Ninayofuraha kukujulisha kuwa mwanao \_\_\_\_\_ amechaguliwa kуjiunga na shule ya sekondari ya wavulana Busokeo. Kuanza masomo ya kidato cha kwanza kwa mwaka 2021, shule ipo umbali wa km 20 kutoka mji mdogo wa Lwangwa ambao ndio makao makuu ya Halmashauri ya Busokelo.

Usafiri ni pikipiki maarufu kwa jila la Bodaboda, Pia unaweza kufika shuleni kupitia mji mdogo wa Katumba. kutoka katumba hadi Isange ni Tsh 4000/= kwa usafiri wa gari (NOAH) . shuka standi ya Isanu, ukishuka panda bodaboda hadi shuleni nauli ni Tsh. 1000 tu. Shule itafunguliwa rasmi tarehe 04/01/2021 siku ya JUMATATU.

Mwisho wa mwanafunzi kuripoti ni saa 10 jion

**2. SARE ZA SHULE**

- i. Suruali (2) za kijivu iliyokolea na mbili za dark blue, zisizo za kubana zenye celebrational na tan up. Zenye kufunika kamba za viatu
- ii. Mashati (2) meupe mikono mifupi yasiyo ya kubana
- iii. Tai (2) za kijivu na ( 2) za dark blue zenye kufika kwenye kitovu
- iv. Sweta (@) rangi ya kijivu iliyokolea yenye muundo wa V-shape. shingoni
- v. Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba vyenye visigino vifupi 2 pair
- vi. Soksi nyeusi pair (3)
- vii. Track suit rangi ya dark blue kwaajili ya michezo
- viii. Jezi za michezo rangi ya blue au nyekundu

- ix. Jacket rangi nyeusi lisilochanganywa rangi
- x. T shirt (2) form six damu ya mzee, zinapatikana shulen i kwa Tsh 10,000/=
- xi. Raba za michezo
- xii. Aje na nguo za ndani za kutosha,taulo

**MUHIMU:**

Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo nyingine za nyumbani tofauti na alizoagizwa hapo juu

**3. MAHITAJI YA BWENINI**

- i. Godoro 1 futi 2  $\frac{1}{2}$  x 6 na mto mmoja pamoja na foronya 2 pink & light blue
- ii. Blanket 1 zito na mashuka (4) mawili rangi ya pink na 2 rangi ya blue bahari
- iii. Sanduku la chuma (trunk)
- iv. Ndoo (2) kwaajili ya kuogea na kufulia
- v. Sabuni za kuogea na kufulia, mafuta ya kupaka, mswaki na dawa ya meno, dawa ya kiatu (kiwi)
- vi. Vyombo vya kulia chakula: sahani, bakuli, kijiko na kikombe
- vii. Mwamvuli (1) rangi yoyote

**4. VIFAA VYA DARASANI**

- i. Daftari kubwa 10 counter book (quire 3)
- ii. Kalamu za wino, pencil, mifuto, vichongeo na rula pamoja na mathematical table (mkebe)
- iii. Graph pad (2) na four figure (1)
- iv. Daftari za mazoezi ndogo (10)
- v. Ream (A4) mbili (2). Moja muhula wa (1) na nyingine muhula wa (2)
- vi. Dictionary (1) English to English
- vii. Saa ya mkononi
- viii. Faili moja kwaajili ya kuhifadhi kumbukumbu zake

**5. VIFAA VYA USAFI**

- i. Jembe (1) lenye mpini, kwanja 1, ufagio aina ya chelewa (1)
- ii. Mopa, squizer pamoja na brush ya kudekia

**MUHIMU**

- ❖ Aje na cheti cha kuzaliwa , picha za pass poti size (4) za rangi
- ❖ Picha za wazazi au walezi watakao mtembelea kila mmoja picha (1) na wasizidi wanne
- ❖ Vifaa vyote vitakaguliwa wakati wa kuripoti
- ❖ Mwanafunzi aje na bima ya afya(pesa Tsh. 20000/= itakabidhiwa shulen i kwaajili ya gharama ya usafiri )

**6. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

- a. Medical examination form ambayo itahitaji mwanafunzi apimwe kikamilifu na kujazwa na mganga wa hospitali ya serikali. Form hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni, form ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki migomo, fujo na makosa ya jinai
- b. Form ya mzazi ya kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa shuleni

**7. GHARAMA ZA HOSTELI**

Gharama za Hosteli kwa mwaka ni 620,000/= aidha fedha hizo zitalipwa kwa awamu nne (4) kwa mchanganuo ufuatao

- A. Awamu I January 250,000/=
- B. Awamu II March 60,000/=
- C. Awamu III July 250,000/=
- D. Awamu IV September 60,000/=

Michano yote ilipwe kupitia Account ya **NMB NO. 63710000903 JINA: SHULE YA SEKONDARY YA WAVULANA BUSOKELO.** Asiyekamilisha michango hatapokelewa shuleni aje na orginal pay shuleni

**KARIBU SHULE YA SEKONDARI YA WAVULANA BUSOKELO (BBSS)**

**ISSAKWISA MWAKILAMA  
KAIMU MKUU WA SHULE**

**TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
SHULE YA SEKONDARI YA WAVULANA BUSOKELO**

**TAARIFA YA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili .....
2. Tarehe ya kuzaliwa .....(tarehe, mwezi mwaka)
3. Kabilia .....Taifa .....
4. Dini madhehebu .....
5. Jina la baba .....Taifa .....
6. Anuani ya baba .....
7. Kazi ya baba.....
8. Jina la mama .....
9. Wazazi wanaishi pamoja au wametengana .....
10. a) Jina na anuani ya mlezi wako kama si mzazi  
.....  
.....  
.....
- b) Kama ni mlezi uhusiano wako naye .....
11. Wakati wa likizo utakuwa kwa nani na wapi ( taja sehemu mha tu utakayokwenda kila wakati na anuani.
12. Nathibitisha kwamba habari zote nilizotoa hapa ni kweli na sahihi .

Sahihi ya mwanafunzi .....

Tarehe .....

Sahihi ya Mzazi .....

Tarehe .....

## **SHULE YA SEKONDARI YA WAVULANA BUSOKELO**

### **FOMU YA KUKUBALI**

#### **FOMU YA KUKUBALI**

##### **1. Sehemu ya mwanafunzi**

Mimi .....  
ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha kwanza mwaka .....

Katika shule ya sekondari ya Wavulana Busokelo na nitafika shulenii bila kuchelewa . ninaahidi kwamba nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na za nchi. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi ya Elimu ya kujitegemea na sitamiliki simu ya mkono wa kushiriki mgono, fujo, na makosa ya jinai kwa muda wote niwapo shulenii.

Anwani yangu ya kudumu ni .....  
.....

##### **2. Sehemu ya Mzazi**

Mimi ..... Ninakubali mtoto  
wangu.....kuchukua nafasi kuingia shule ya sekondari Wavulana Busokelo kidato cha kwanza mwaka .....  
Nina ahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kuijunga na shule. Ninakuhakikisha kuwa nitashirikiana na shule wakti wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na Taifa, na hatamiliki simu ya mkononi awapo shulenii wala kushiriki katika mgomo , fujo na makosa ya jinai kwa muda wote atapokuwa mwanafunzi.

Anuani yangu ya kudumu ni :

.....  
.....

Simu Na .....

Iwapo nitapata uhamisho au kubadilisha makazi, ni lazima nitaijulisha shule kwa maandishi

Sahihi ..... Tarehe .....

## **MEDICAL CERTIFICATE FORM**

STUDENT NAME.....

To be completed by a Government Medical Officer or a doctor from a recognized health institution in respect of form one entrant. Please examine the above as to her/his physical and mental fitness as a student at this school.

The examination should have to involve the following categories

1. Vision with glasses right ..... left.....
2. Blood pressure .....
3. Hemoglobin .....
4. F. V. Bleeding .....
5. Urine for sugar. .....
6. Stool for routine examination .....
7. Venereal diseases .....
8. Neurosis .....
9. T. B. Test .....
10. Any abnormality
  - a) Heart .....
  - b) Lung .....
  - c) Spleen .....
  - d) Chest .....
11. Is there any serious disease e.g. Leprosy, Epilepsy, Asthma,  
Diabetes .....

Doctor's name.....

Signature and official stamp

.....

Date .....

## **SHERIA ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Sheria hizo ni kama ifuatavyo:

1. Heshima na adabu kwa Viongozi, Wazazi, Wafanyakazi, Wanafunzi wengine na Jamii kwa ujumla.
2. Utii kwa Walimu, Wafanyakazi wasio Walimu na Viranja.
3. Kuwahi kufika Shuleni na kutoondoka Shuleni kabla ya Shule kufungwa.
4. Kuzingatia ratiba ya shughuli za kila siku za Shule.
5. Kuwahi katika kila wito (utii kwa kengele).
6. Kuвая sare ya Shule madarassani, muda wa kazi na michezo.
7. Ni marufuku kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa.
8. Hairuhusiwi kutembelea vilabu vya pombe, majumba ya starehe wala njumba ya wageni.
9. Ulevi wa aina yeyote ni marufuku.
10. Ugomvi na matusi ni mwiko.
11. Wizi, kuharibu mali/ kifaa cha Shule au kuandika maandishi na michoro kwenye kuta za shule, milango n.k ni marufuku.
12. Kila mwanafunzi anatakiwa awe msafi.
13. Ni mwiko kutupa taka/ karatasi au uchafu ovyo.
14. Urafiki wa kimapenzi hauruhusiwi Shuleni.
15. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuoa au kuolewa.
16. Ni marufuku kwa mwanafunzi kwenda nyumbani kwa Wafanyakazi bila ruhusa.
17. Ni marufuku kwa mwanafunzi kutumia vyombo vya umeme Bwenini/ darasani au mahali popote ndani ya Shule.
18. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na Simu ya mkononi Shuleni, Adhabu kali itatolewa ikiwemo kulipia uharibifu wa Mfumo wa Umeme na Mzazi kumhamisha Mwanafunzi husika.

## **MIIKO MAALUMU:**

### **MAKOSA YA FUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE.**

- a) Kashfa ya aina yoyote kwa Taifa kama kudharau mambo ya Kitaifa (sikukuu za Kitaifa, mikutano, wimbo wa Taifa, maandalamano, nk.)
- b) Wizi (kuiba).
- c) Kuoa au Kuolewa.
- d) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- e) Kutohudhuria Shule kwa muda mrefu (utoro) bila taarifa.
- f) Kupigana au Kupiga.
- g) Kuchochea ghasia/ kugoma au kuongoza migomo na kuvunja amani na usalama wa shule au watu.
- h) Kuvuta sigara, kunywa pombe, bangi au dawa za kulevyta.
- i) Kuendesha magendo au ulanguzi wa aina yoyote.
- j) Kosa la jinai, kosa likithibitishwa na polisi, au mahakamani.
- k) Kulala nje ya shule bila ruhusa.
- l) Kugoma adhabu.
- m) Kuwa na simu ya mkononi Shuleni.
- n) Ubakaji.
- o) Kumpa mimba msichana ndani au nje ya shule.